

HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA

(BaruazotezakiofisizitumwekwaMkurugenziMtendaji)

Mkoa wa Arusha,
Telegram: Arusha
Simu: 027 250 2737
Mobile Na. 073 65000476
Fax: 250 3701
Email:ded@arushadc.go.tz
Tovuti:www.arushadc.go.tz



UkumbiwaWilaya
S.L.P.2330
ARUSHA

10/201/2019.

MIRADI INAYOTEKELEZWA KATIKA HALMASHAURI YA ARUSHA KWAMWAKA WA FEDHA 2017/2018 & 2018/2019.

Halmashauri ya Arusha inatekeleza miradi mbalimbali katika kata zote 27. Katika kuhakikisha huduma za jamii zinapatika kwa urahisi kwa urahisi katika uwiano sawa wa maeneo ya miji na vijiji, Halmashauri imejikita kuelekeza nguvu katika kutekeleza miradi katika sekta za Elimu, Afya, Maji, Mazingira, Kilimo, Mifugo na Ardhi.

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018-2018/2019, Halmashauri inaendelea kutekeleza miradi mipya fedha pamoja na miradi bakaa inayoendelea kutoka mwaka wa fedha uliopita 2015/2016 na mwaka wa fedha 2016/2017.

Kadhalika halmashauri inatekeleza miradi yake kwa kuzingatia zaidi ushirikishwaji wa serikali, wananchi na wadau wa maendeleo ndani na nje ya Tanzania.

Halmashauri pia inahakikisha miradi hiyo inazingatia weledi ikiwemo usimamizi thabiti wa matumizi ya fedha na utekelezaji unaozingatia thamani halisi ya fedha kwa kulinganisha na ubora wa mradi.

Miradi inayotekelezwa ni miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Vyumba vya Madarasa, Nyumba za walimu, Bwalo, hosteli pamoja na vyoo vya wanafunzi katika shule za Msingi na Sekondari, Ujenzi na Ukarabati wa Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali pamoja na ujenzi wa nyumba za wahudumu wa Afya ikiwemo madaktari na wauguzi, Ujenzi na Ukarabari wa miundombinu ya barabara pamoja na vivuko, madaraja na mitaro ya kupitisha maji kwenye kingo za barabara.

Muonekano wa Miradi inayotekelezwa katika Picha:-

MRADI WA UJENZI WA ZAHANATI YA MANYIRE.

Mradi wa Ujenzi wa Zahanati ya Manyire ulianza rasmi mwaka 2010 na kufikia boma, mwaka 2018 ubalozi wa Japani nchini Tanzania ulitoa fedha kiasi cha shilingi milioni 191 kwa ajili ya umaliziaji wa majengo hayo.

Mradi huu ukikamilika yataombewa kibali na kusajiliwa kuwa Kituo cha Afya.



MUONEKANO WA JENGO LA KITUO CHA AFYA MANYIRE.



MAJENGO YA KITUO CHA AFYA MANYIRE



MRADI WA UJENZI WA SHULE MPYA YA SEKONDARI MANYIRE.

Mradi wa Ujenzi wa Shule mpya ya sekondari Manyire ulianza rasmi mwishoni mwa mwaka 2018.

Fedha za mradi huu zimetokana na fidia ya shamba la kijiji walililowapa Chuo kuku Mzumbe kiasi cha shilingi milioni 400.

Mradi huu umehusisha ujenzi wa vyumba vine vya madarasa na ofisi za wali-



UJENZI WA VYUMBA VIWILI VYA MADARA SHULE YA MSINGI MUSA KATA YA MUSA

Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na ofisi ndogo ya walimu shule ya Msingi Musa umejengwa kwa Ufadhili wa kampuni ya kitalii ya Tanzania Big Game Safaris Ltd. umegharimu shilingi million 53.



MRADI WA UJENZI WA KITUO CHA AFYA MBUYUNI.

Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya Mbuyuni kata ya Oljoro ulianza rasmi mwishoni mwa mwaka 2018.

Fedha za mradi huu zimetolewa na serikali kupitia mpango wake wa kuboresha miundombinu ya vituo vya Afya nchini kiasi cha shilingi milioni 400 zilitolewa.

Mradi huu umehusisha ujenzi wa maabara, jengo la mama na mtoto, Chumba cha kupasulia pamoja na nyumba ya mganga.



MAJENGO YA KITUO CHA AFYA MBUYUNI KATA YA OLJORO



MRADI WA UJENZI WA NYUMBA YA MTUMISHI WA AFYA

Mradi wa Ujenzi wa nyumba ya mtumishi wa afya, kituo cha Afya Mbuyuni
kata ya Oljoro ulianza rasmi mwishoni mwa mwaka 2018.

Fedha za mradi huu zimetoklewa na serikali kupitia mpango wa kuboresha
vituo vya afya.



MRADI WA UJENZI SHULE YA SEKONDARI LOSIKITO

Mradi wa Ujenzi wa Shule mpya ya sekondari Losikiti kata ya Mwandeti, ulianza rasmi mwa mwaka 2018 na kukamilika.

Fedha za mradi huu nguvu za wananchi wa kijiji cha Losikito, mradi umegharimu kiasi cha shilingi milioni 320.

Mradi huu umehusisha ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa na ofisi za walimu pamoja na vyoo vya walimu na wanafunzi, maabara na nyumba ya walimu yenye shemu ya kuishi familia tatu (3 in 1).



UJENZI WA MAABARA SHULE YA SEKONDARI LOSIKITO



VYOO VYA WANAFUNZI SHULE MPYA YA SEKONDARI LOSIKITO



UJENZI WA NYUMBA YA WALIMU LOSIKITO
Nyumba ya walimu yenye sehemu tatu (3 in 1) shule ya
sekondari Losikito



MRADI WA UJENZI SHULE MPYA YA SEKONDARI OLDONYOWAS

Mradi wa Ujenzi wa Shule mpya ya sekondari Oldonyowas kata ya Oldonyowas ulianza rasmi mwa mwaka 2018 na kukamilika kwa baadhi ya majengo mwaka 2019.

Fedha za mradi huu zimetokana na nguvu za wananchi wa kijiji cha Oldonyowas, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii -TASAF PAMOJA NA Mmlaka ya Hifadhi ya Taifa TANAPA. umegharimu kiasi cha shilingi milioni 320.

Mradi huu umehusisha ujenzi wa Jengo la Utawala, vyumba nane vya madarasa na ofisi 2 ndogo za walimu, pamoja na vyoo vya walimu na wanafunzi, Jengo la Maabara na nyumba ya walimu yenye shemu ya kuishi familia mbili (2 in 1).



JENGO LA UTAWALA SHULE MPYA YA SEKONDARI OLDONYOWAS

Jengo la Utawala shule ya Sekondari Oldonyowas limejengwa kwa gharama ya Tsh. 92, 187,107.00, jengo hilo litajumuisha ofisi ya mkuu wa shule, Ofisi ya walimu walimu wote, pamoja na maliwato



UJENZI WA JENGO LA UTAWALA SHULE YA SEKONDARI OL-DONYOWAS LIMEJENGWA KUPITIA MRADI WA TASAF



**UJENZI WA VYUMBA VIWILI VYA MADARA SHULE YA
SEKONDARI OLDONYOWAS.**

Ujenzi wa vyumba viwili vya madarsa shule ya Sekondari
Oldonyowas umefanyika kupitia Mradi wa TASAF.



UJENZI WA MAABARA SHULE YA SEKONDARI OLDONYOWAS.

Ujenzi wa Maabara shule ya Sekondari Oldonyowas umefanyika kwa mchango mkubwa na jitihada za wananchi wa Oldonyowas , ujenzi utakaogharimu kiasi cha shilingi milini 40



MUONEKANO WA JENGO LA MAABARA SHULE YA SEKONDARI
OLDONYOWAS



UJENZI WA NYUMBA YA WALIMU SHULE YA SEKONDARI OLDONYOWAS.

Ujenzi wa nyumba ya walimu yenye sehemu ya kuishi familia mbili
(2 in 1) shule ya Sekondari Oldonyowas mradi umefanyika kupitia
Mradi wa TASAF.



UJENZI WA VYOO VYA WALIMU NA WANAFUNZI SHULE



**WANAFUNZI WA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2019 WAKI-
WA KWENYE VYUMBA VIPYA VYA MADARASA SHULE YA
SEKONDARI OLDONYOWAS.**



**MRADI WA UJENZI WA JENGO LA MAMA NA MTOTO
(MATERNITY WARD) HOSPITALI YA WILAYA YA OLTURUMET.**

Ujenzi unategemea kugharimu kiasi cha shilingi Milioni 147

Fedha za Fidia ya deni la shamba la Lakilaki.



MUONEKANO WA JENGO LA MAMA NA MTOTO
(MATERNITY WARD) HOSPITALI YA WILAYA YA OLTURU-
MET.



**MRADI WA UJENZI WA JENGO LA KUHIFADHIA CHANJO
HOSPITALI YA WILAYA OLTURUMET.**

Ujenzi wa jengo la stoo ya Chanjo hospitali ya Olturumet
ujenzio utakaogharimu kiasi cha shilingi milioni 45.



MRADI WA MAJI BWAWANI.

Mradi wa maji Bwawani ni moja ya miradi ya vijiji kumi, iliyoanza kutekelezwa mwaka 2012 kwa gharama ya **Tsh. 1,119,525,354.75**, mpaka sasa mradi bado unaenedelea. Mradi huo umehusisha ujenzi wa nyumba ya mashine na pump, usambazaji wa mabomba, ujenzi wa matank ya juu ya kuhifadhia maji yenye ujazo wa mita za ujazo 80,40, vituo 26 vya kuchotea maji, malambo 2 ya kunyweshea mifugo, pamoja na miundombinu ya kuvunia maji yenye mita za ujazo 5,3,1.



MRADI WA MAJI LOOVILUKUNY

Mradi wa maji Loovilukuny ni moja ya miradi ya vijiji kumi, iliyoanza kutekelezwa mwaka 2012 kwa gharama ya **Tsh. 1,035,300,797.00**. mpaka sasa umekamilika kwa asilimia 95%, mpaka sasa umekamilika kwa asilimia 95% mradi umehusisha ujenzi wa nyumba ya mashine na pump, usambazaji wa mabomba, ujenzi wa matank 3 ya kuhifadha maji yenye mita za ujazo 160, vituo 19 vya kuchotea maji, malambo 2 ya kunyweshea mifugo, pamoja na miundombinu ya kuvunia maji. Yenye mita za ujazo 5,3,1.



MRADI WA UJENZI WA MFREJI OLEVOLOSI KATA YA KIMNYAKI.

Mradi wa ukarabati wa ujenzi wa Mfereji wa Umwagiliaji Olevolosi, ulianza mwaka 2018 na umefanyika kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF awamu ya III. Mpaka kukamilika mradi utagharimu kiasi cha **Tsh. 71,101,587.50**, Mradi huu unalenga kutoa ajira za muda kwa Kaya zilizo kwenye Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini.



MRADI WA UJENZI WA MFREJI OLEVOLOSI KATA YA KIMNYAKI.

Wanufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini wakipanda miti kwa ajili ya Utunzaji wa Mazingira katika Mfereji wa Olev olosi, Mradi huu unategemea kuwaongezea kipato wanakaya hao.



MRADI WA UJENZI WA ZAHANATI YA MIDAWWE KATA YA BANGATA.

Mradi wa ujenzi wa Zhanati Midawe kata ya Bangata, ulianza mwaka 2017/18 na umefanyika kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF awamu ya III. Mpaka kukamilika mradi utagharimu kiasi cha Tsh. 70,150,400.00, hata hivyo baada ya kukamilika halmashauri inategemea kuisajili kama kituo cha Afya cha Kata ya Bangata.



MRADI WA UJENZI WA NYUMBA YA WALIMU YENYE SHEHEMU MBILI (2 IN 1)

Ujenzi wa yumba ya walimu shule ya msingi Engikaret kata ya Bangata, mradi unaotekelezwa na Mfuko wa Hifadhi ya jami TASAF awamu ya III kwa gharama ya Tsh. 50,056,270.00,.



MRADI WA UJENZI WA SHULE YA SEKONDARI SAMBASHA.

Mradi wa Ujenzi wa vyumba viwili vya madaras na choo cha wanafunzi cha matundu sita, shule ya sekondari Sambasha umetekelezwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii -TASAF awamu ya III.

Ujenzi huu umegharimu kiasi cha shilingi milioni 74.3, umekamilika kwa asilimia 100.



MRADI WA UJENZI WA SHULE YA SEKONDARI SAMBASHA.

Choo cha wanafunzi chenye matundu sita, shule ya sekondari Sambasha, Mradi umetekelezwa mwaka wa fedha 2017/2018 kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii -TASAF awamu ya III.



MRADI WA UJENZI WA NYUMBA YA WALIMU SHULE YA MSINGI MUNGUSHI.

Mradi wa Ujenzi wa nyumba ya walimu yenye sehemu ya kuishi familia mbili (2 in 1) shule ya Msingi Mungushi kata ya Bwawani, Mradi huu ume-tekelezwa katika mwaka wa fedha 2017/2018, kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii -TASAF awamu ya III, kwa gharama ya shilingi milioni 70.



Imeandaliwa na;
Kitengo cha Habari.
Halmashauri ya Wilaya ya Arusha.
S.L.P 2330,
ARUSHA.
Barua pepe: ded@arushadc.go.tz
Tavuti: www.arushadc.go.tz
Facebook page: Arusha District Council